Nia Dhidi ya Injili – Je Unaionea Haya?

(Attitude Towards The Gospel – Are You Ashamed of it?)

Na

Ellis P. Forsman

Nia Dhidi ya Injili – Je Unaionea Haya?

Na

Ellis P. Forsman

Septemba 16, 2015

Nia Dhidi ya Injili – Je Unaionea Haya?

Rum. 1:14-17

Nia njema kimsingi ni muhimu. Ni muhimu kwa umoja katika kusanyiko la sehemu Fulani.

Nia hutafsiriwa kama: Ni hali ya akili au hisia, kuwa katika hali isio sawa.

Kwa maneno mengine, ni hali ya mtu kutambua kitu.

Kidini tunaweza kuwa na nia inayoleta baraka toka kwa Mungu, au inayoleta kutokupendelea toka kwake. Tulijifunza kuhusu nia zetu dhidi ya Mungu na Yesu Kristo, sasa tutajifunza kuhusu nia zetu dhidi ya injili.

Nia Dhidi Ya Injili

Leo hii inatangazwa na waalimu wa dini kwamba ukweli ni kitu kinachofanana, na haiwezi kueleweka. Wanafikiri ni upumbavu kuishi kulingana na neno la Mungu na wanawaita "wahalalishi" wanaojaribu kufuata neno la Mungu.

1 Kor. 1:18-21, "*Kwa sababu neno la msalaba kwao wanaopotea ni upuuzi, bali sisi tunaookolewa ni nguvu ya Mungu. Kwa kuwa imeandikwa nitaiharibu hekima yao wenye hekima, na akili zao wenye akili nitazikataa. Yu wapi mwenye hekima? Yu wapi mwandishi? Yu wapi mlete hoja wa zamani hizi? Je? Mungu hakuifanya hekima ya dunia kuwa ni upumbavu. Kwa maana katika hekima ya Mungu dunia isipopata kumjua Mungu kwa hekima yake, Mungu alipenda kuwaokoa waaminio kwa upuuzi wa lile neno linalohubiriwa.*"

Kabla Yesu hajapaa kwenda mbinguni, alieleza nia hii kwa wale ambao hawakumuelewa, au wale ambao hawakutaka kumuelewa.

Yoh. 8:43-44, "*Mbona hamyafahamu hayo niyasemayo? Ni kwa sababu ninyi hamwezi kulisikia neno langu. Ninyi ni wa baba yenu Ibilisi na tama ya baba yenu ndizo mpendazo kuzitenda. Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo, wala hakusimama katika kweli kwa kuwa hamna hiyo kweli ndani yake. Asemapo uongo husema yaliyo yake mwenyewe; kwa sababu yeye ni mwongo na baba wa huo.*"

Yoh. 8:37, "*Najua ya kuwa ninyi ni uzao wa Ibrahimu lakini mnatafta kuniua kwa sababu neno langu halimo ndani yenu.*"

Walichagua kuamini kuwa wangeokolewa kwa sababu tu walikuwa uzao wa Ibrahimu, hivyo wakazembea kuhusu Sheria ya Musa.

Walitaka njia rahisi kwenda mbinguni. Labda hawakutaka kusikiliza kitu kingine kipya. Na viongozi wa Kiyahudi hawakutaka kuachia nafasi zao za uongozi.

Viongozi wa dini wa ulimwengu huu wana madai kwamba Biblia haieleweki siku hizi, kwamba inahitaji "maboresho" irudi kuwa mpya na kuibadilisha ulimwengu. Hivyo, wanafundisha injili ya jamii.

Pia wanatafuta njia yao rahisi na bado wana mshtuko unawangojea siku ya Hukumu, pia.

Wanapenda kuitwa majina na kuita ye yote anayejaribu kuishi kulingana na maandiko kuwa "hana elimu". Wanajiita wanafunzi wa Biblia, ala bado wao wenyewe wanakiuka neno la Mungu. Wanajipa "majina" ya kidini na hukasirika kama hutumii majina haya (kama vile Mteule, Baba, n.k).

Mat. 23:9, "*Wala msimwite mtu baba duniani; maana Baba yenu ni mmoja, aliye wa mbinguni.*"

Wengine wanajivunia umahiri na elimu yao waliyohitimu, lakini bado hukiuka pale linapokuja swala la kujua kile anachokitaka Mungu.

Badala yake wanahubiri kile ambacho watu wanapenda kusikia. Paulo alisema:

- Gal. 1:10, "*Maana sasa je! Ni wanadamu ninaowashawishi, au Mungu? Au nataka kuwapendeza wanadamu au Mungu? Au nataka kuwapendeza wanadamu? Kama ningekuwa hata sasa nawapendeza wanadamu, nisingekuwa mtumwa wa Kristo.*"
- 1 Kor. 9:16, "*Maana ijapokuwa naihubiri injili, sina la kujisifia maana nimewekewa sharti; tena ole wangu nisipoihubiri injili.*"

Kwa nini ni tofauti leo? Kwa nini leo hii watu hawasikii ole ambayo Paulo anaisema wanaposhindwa kuihubiri injili?

Yohana alifundisha kuhusu umuhimu wa neno la Mungu. 2 Yoh. 1:9-11, "*Kila apitaye cheo wala asidumu katika mafundisho ya Kristo, yeye hana Mungu. Yeye adumuye katika mafundisho hayo, huyo ana Baba na Mwana pia. Mtu akija kwenu naye haleti mafundisho hayo, msimkaribishe nyumbani mwenu, wala msimpe salamu. Maana yeye ampaye salamu huzishiriki kazi zake mbovu.*"

Ulimwengu wa dini haupendi neno “Mafundisho”. Kwao neno hili ni chafu. Wanataka kila mtu awe nao ili wasihubiri injili nyingine ambayo inaweza kumkwaza mtu.

Bado, Yohana anasema tusipokaa katika mafundisho ya Kristo, Mungu hayupo ndani mwetu.

Paulo aliwaonya ndugu wa Galatia wasichanganye chochote isipokuwa neno la Mungu. Gal. 1:7-9, “*…Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaaniwe. Kama tulivyotangulia kusema na sasa nasema tena, mtu ye yote akiwahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo mliyoipokea, na alaaniwe.*”

Kuacha mafundisho ya Kristo ni kuhubiri injili nyingine.

Tunapaswa kujaribu kila kitu tunachokisikia ili kuona kama ni neno la Mungu. 1 Yoh. 4:1, “*Wapenzi msiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho kwamba zimetokana na Mungu; kwa sababu manabii wa uongo wengi wametokea duniani.*”

Kama haiwezi kupatikana kwenye Biblia, ikatae.

Wakati Fulani nilimsikia mwana dini akimwambia mwenzake ambaye hakukubaliana naye, kwamba alikuwa mtu mwenye elimu ya neno la Mungu hivyo hapaswi kutiwa changamoto kwa chochote anachofundisha na mtu ye yote yule. Ni ukengeufu wa aina gani!

Hakutaka tu kuonyeshwa kwamba alikuwa na kosa, hivyo alishambulia ujuzi wa wengine na tabia.

2 Tim. 2:15, “*Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli.*”

Nia Ya Paulo Dhidi Ya Injili

Paulo alipoanza waraka wake kwa Warumi, aliandika kuhusu hamu yake ya kutaka kuwaona.

Angalia maombi yake yenye juhudi dhidi yao. Rum. 1:9-10, “*Kwa maana Mungu nimwabuduye kwa roho yangu katika injili ya Mwana wake, ni shahidi wangu jinsi niwatajavyo pasipo kukoma, siku zote katika sala zangu, nikiomba nije kwenu hivi karibuni, Mungu akipenda kuifanikisha safari yangu.*”

Hakutaka mafanikio binafsi kifedha; aliwataka wale waliokuwa Rumi kufanikiwa katika ujuzi wa neno la Mungu.

Alikuwa na hamu ya kuwatia moyo kupitia elimu njema. Rum. 1:11-12, “*Kwa maana ninatamani sana kuwaona, nipate kuwapa karama ya rohoni ili mfanywe imara; yaani tufarijiane mimi na ninyi kila mtu kwa imani ya mwenzake, yenu na yangu.*”

Alipanga kuwatembelea ili kwamba aweze kuwa na mataunda miongoni mwao. Rum. 1:13, "*Lakini ndugu zangu sipendi msiwe na habari ya kuwa mara nyingi nalikusudia kuja kwenu nikazuiliwa, hata sasa, ili nipate kuwa na matunda kwenu ninyi pia kama nilivyo nayo katika mataifa wengine.*"

Hapana Paulo alikuwa haongelei kuhusu kuchukua matunda. Bali alikuwa anazungumzia majibu yatakayopatikana baada ya kuwahubiria injili – kwamba baadhi au wengi wao watatii injili ya Kristo aliyowahubiri.

Hamu yake ya kutaka kuwaona ilihusiana na injili.

Aliyotumika kama Mtume wa Kristo. Rum. 1:1, "*Paulo Mtumwa wa Kristo Yesu, aliyeitwa kuwa mtume na kutengwa aihubiri Injili ya Mungu;*"

Ambayo hakuionea haya. Rumi. 1:16, "*Kwa maana siionei haya injili, kwa sababu ni uwezo wa Mungu uuletao wokovu kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza na kwa Myunani pia.*"

Je tumewahi kuionea haya injili ya Kristo? Je tuna aibu ya kuwaambia wengine kuhusu Yesu?

Hii yaweza kuwa sababu ya wengine kutofanya vyema katika uinjilisti wao binafsi?

Nia yetu ni nini kuhusu injili ya Kristo?

Labda kwa uchunguzi wa jinsi gani na kwa nini Paulo hakuionea haya injili, tunaweza kuwa na juhudi katika jitihada zetu za kushiriki habari njema ya Yesu Kristo na wengine.

Paulo Hakuionea Haya Injili

Hakuona haya kuvipi...

Alijisikia kwamba anawajibika kuihubiri injili kwa kila mmoja. Kwa Wayahudi na Wayunani pia (wasio Wayahudi, kwa wenye hekima na wasio na hekima. Rum. 1:14, "*Nawiwa na Wayunani na wasio Wayunani nawiwa na wenye hekima na wasio na hekima.*"

Jukumu lake la kuhubiri kwa sehemu ilikuwa upendeleo kutoka kwa Mungu. 1 Kor. 15:9-10, "*Maana mimi ni mdogo katika mitume nisiyestahili kuitwa mitume, kwa sababu naliliudhi kanisa la Mungu. Lakini kwa neema ya Mungu nimekuwa hivi nilivyo; na neema yake iliyo kwangu ilikuwa si bure, bali nalizidi sana kufanya kazi kupita wao wote; wala si mimi bali ni neema ya Mungu pamoja name.*"

Hakika Paulo alijisikia vibaya kwa kile alichowafanyia Wakristo. Alijisikia kuwa hakufaa kuwa mtume; bali kwa sababu ya neema

ya Mungu katika kumsaidia akumbuke makosa yake, alijisikia kwamba anapaswa kufanya kazi kwa nguvu kwa ajili ya Bwana ili kurekebisha kile alichokifanya.

Yesu alimchagua kuwa mtume, hivyo alijisikia kuwa na jukumu la kutimiza wajibu huo. Alishukuru kwa nafasi ambayo Mungu alimpa kufanya kazi katika huduma ya kufundisha injili ya Kristo. 1 Tim. 1:12-14, "*Nami namshukuru Kristo Yesu Bwana wetu, aliyenitia nguvu kwa sababu aliniona kuwa mwaminifu, akaniweka katika utumishi wake; ingawa hapo kwanza nalikuwa mtukanaji, mwenye kuudhi watu, mwenye jeuri lakini nalipata rehema kwa kuwa nalitenda hivyo kwa ujinga, na kutokuwa na imani. Na neema ya Bwana wetu ilizidi sana, pamoja na imani na upendo lililo katika Kristo Yesu.*"

Paulo alikuwa tayari kuhubiri injili Rumi. Nafasi yo yote aliyopewa aliitumia! Rum. 1:15, "Warumi 1:15, "*Kwa hiyo kwa upande wangu mimi ni tayari kuihubiri injili hata na kwenu ninyi mnaokaa Rumi.*"

Hata ivyo alijua kwamba maisha yake yangeishia Rumi.

Paulo alionyesha kwamba hakuona haya kwa utayari wake na maandalizi ya kuihubiri injili wakati wo wote na mahali popote!

Kwa nini hakuona haya.

Ni uwezo wa Mungu uuletao wokovu kwetu sote. Rum. 1:16, "*Kwa maana siionei haya injili kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza na kwa Myunani pia.*"

Nashangaa ninapo sikia watu wanasema, "Usinihubirie!"

Yesu aliwaambia wanafunzi wake kuhubiri kutoka kwenye paa za nyumba.

- Mat.10:27, "*Niwaambialo ninyi katika giza, lisemeni katika nuru, na msikialo kwa siri lihubirini juu ya nyumba.*"
- Mk. 16:15-16, "*Akawaambia enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka asiyeamini atahukumiwa*"
- Mdo. 5:42, "*Na kila siku ndani ya hekalu na nyumbani mwao, hawakuacha kufundisha na kuhubiri habari njema za Yesu kwamba ni Kristo.*"
- Rum. 10:15, "*Nasema kama na watu wenye akili, lifikirini ninyi ninenalo.*"

- 2 Tim. 4:2, "*Lihubiri neno uwe tayari wakati ukufaao na wakati usiokufaa, karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho.*"

Hapana, sio rahisi kila mara kutangaza neno la Mungu wakati walio wengi katika ulimwengu hawako tayari kukubali mtu anapowafundisha neno la Mungu.

Vilevile, ni agizo la Mungu kwetu kuhubiri injili na ni uwezo wake kuokoa. Kuna nafsi nje pale ambazo zimeiva kwa ajili ya neno la Mungu kufundishwa kwao. Watapotea kama tusipowafikia.

Hubiri injili kwa maana inaeleza kuhusu Kristo, uweza wa Mungu na hekima ya Mungu. 1 Kor. 1:23-24, "*Bali sisi tunamhubiri Kristo aliyesulubiwa; kwa Wayahudi ni kikwazo na kwa Wayunani ni upuuzi, bali kwao waitwao Wayahudi kwa Wayunani, ni Kristo nguvu ya Mungu na hekima ya Mungu.*"

Paulo hakuona haya kuhubiri injili kwa sababu inafunua haki ya Mungu katika wokovu.

Jinsi wenye haki wataishi kwa imani. Rum. 1:17, "*Kwa maana haki ya Mungu inadhihirishwa ndani yake toka imani hata imani; kama ilivyoandikwa mwenye haki ataishi kwa imani.*"

Paulo hakuona aibu kuhubiri injili kwa sababu ya uwezo wake na ujumbe. Hakuona haya kuhubiri injili kwa ye yote aliyependa kusikia!

Kutoka kwa Paulo tunaweza kuona sababu tofauti ni kwa nini…

Hatupaswi Kuionea Haya Injili

Injili inabaki vile vile. Bado ni uwezo wa Mungu kuokoa. Bado ni uwezo unaozalisha imani katika mioyo ya wale wanaosikia. Rum. 10:17, "*Basi imani chanzo chake ni kusikia na kusikia huja kwa neno la Kristo.*"

Bado ni uwezo unazalisha matunda kwa wale wanao sikia na kufahamu ukweli. Kol. 1:5-6, "*Kwa sababu ya tumaini mlilowekewa akiba mbinguni, ambalo habari zake mlizisikia zamani kwa neno la kweli ya injili, iliyofika kwenu kama ilivyo katika ulimwengu wote, na kuzaa matunda na kukua kama inavyokuwa kwenu pia, tangu siku mlipoisikia mkaifahamu sana neema ya Mungu katika kweli,*"

Bado inafunua haki ya Mungu katika wokovu; jinsi Yesu alivyozifia dhambi zetu. 1 Kor. 15:1-4, "*Basi ndugu zangu nawaarifu ile injili niliyowahubiri, ambayo ndiyo mliyoipokea na katika hiyo mnasimama, na kwa hiyo mnaokolewa, ikiwa mnayashika sana maneno niliyowahubiri isipokuwa mliamini bure. Kwa maana naliwatolea ninyi hapo mwanzo yale niliyoyapokea mimi*

mwenyewe ya kuwa Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo maandiko; na ya kuwa alizikwa na ya kuwa alifufuka siku ya tatu, kama yanenavyo maandiko;"

Bado inafunua jinsi tunavyoweza kupata msamaha wa dhambi katika Yesu kupitia imani, toba na ubatizo. Mdo. 2:36-38, "*Basi nyumba yote ya Israeli na wajue yakini ya kwamba Mungu amemfanya Yesu huyo mliyemsulubisha kuwa Bwana na Kristo. Walipoyasikia wakachomwa mioyo yao wakamwambia Petro na mitume wengine tutendeje ndugu zetu? Petro akawaambia tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo mpate ondolea la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*"

Ndugu na dada, kupita kwa wakati hakuja dhoofisha uwezo na ujumbe wa injili ya Kristo!

Hitaji linabaki pale pale. Nafsi bado ziko katika hitaji la kuokolewa.

Wote wametenda dhami. Rum. 3:23, "*Kwa maana wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu;*"

Mshahara wa dhambi ni mauti. Rum. 6:23, "*Kwa maana mshahara dhambi ni mauti, bali karama ya Mungu ni uzima wa milele kwa Mwanawe Yesu Kristo Bwana wetu.*"

Kwa wenye hekima na wapumbavu, walioko mbali na walioko karibu. Yesu bado ni njia ya kwenda kwa Baba kwa watu wote. Yoh. 14:6, "*Yesu akamwambia mimi ndimi njia na kweli na uzima; **mtu hadi** kwa Baba ila kwa njia ya mimi.*"

Injili yake bado inahitaji kuhubiriwa kwa kila kiumbe. Mk. 16:15-16, "*Akawaambia enendeni ulimwenguni mwote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aamniniye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa.*"

Kupita kwa muda hakuja toa tiketi kwa injili ya Kristo kutokuhubiriwa!

Kutoka katika mfano wa Paulo, tunaweza kufahamu nia njema na tabia ambayo tunatakiwa kuwa nayo katika kuhubiri injili ya Kristo.

Wale Wasioionea Haya Injili Watakuwa Na Shauku Na Dhamira Ya Jukumu Hilo...

Kwa Mungu aliyewaokoa.

Je hatuna shukrani kwa kile ambacho Mungu ametutendea? Je hii haita badilisha mwenendo wa maisha yetu? Gal. 2:20, "*Nimesulubiwa pamoja na Kristo lakini ni hai, wala si mimi tena bali*

Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda akatoa nafsi yake kwa ajili yangu."

Tunapaswa kuwa na hisia ya jukumu kwa wale waliopotea.

Je hatujali kuhusu maisha yao ya milele na wafe katika dhambi zao? Je hii haitatusukuma kufanya kitu fulani?

2 Kor.5:11, "*Basi tukiijua hofu ya Bwana twawavuta wanadamu; lakini tumedhihirishwa mbele za Mungu. Nami natumaini kuwa tumedhihirishwa katika dhamiri zenu pia.*"

Wale wasioionea haya injili wataona jukumu kama hili la Paulo. Rum. 1:14, "*Nawiwa na Wayunani na wasio Wayunani, nawiwa na wenye hekima na wasio na hekima.*"

Wale Wasioionea Haya Injili Watajiandaa...

Kushiriki injili kadiri wapatavyo nafasi.

Kama hatuna hakika tuseme nini, watajifunza (na kurudia kujifunza).

- 1 Pet. 3:15, "*Mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu.*"
- Heb. 5:12, "*Kwa maana iwapasavyo kuwa waalimu maana wakati mwingi umepita, mnahitaji kufundishwa na mtu mafundisho ya kwanza ya maneno ya Mungu; nanyi mmekuwa mnahitaji maziwa wala si chakula kigumu.*"

Wale waliojiandaa hawata pumzika hadi watafute njia ya kuwasilisha injili kwa wengine. Alafu watakuwa wanatarajia "mlango ulio wazi" ili wafundishe wengine.

1 Kor.3:5, "*Basi Apolo ni nani? Na Paulo ni nani? Ni wahudumu ambao kwao mliamini; na kila mtu kama Bwana alivyompa.*"

Sawa na Wakristo wa kwanza, tunajukumu la kutangaza injili kadiri tupatapo nafasi.

Rum. 10:14-15, "*Basi wamwiteje yeye wasiyemwamini? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikieje pasipo mhubiri? Tena wahubirije, wasipopelekwa? Kama ilivyoandikwa ni mizuri kama nini miguu yao wahubirio habari ya mema.*"

Wengine wenu mnaweza kujiona kuwa hamfai kufundisha, lakini bado mnaweza kuwaalika. Mdo. 10:24, "*Siku ya pili yake*

wakaingia Kaisaria. Na Kornelio alikuwa akiwangojea, hali amekusanya jamaa zake na rafiki zake."

Wale ambao hawaionei haya injili watakuwa tayari kama Paulo. Rum. 1:15, "*Kwa hiyo kwa upande wangu mimi ni tayari kuihubiri injili hata na kwenu ninyi mkaao Rumi.*"

Hitimisho

Je unaionea haya injili ya Kristo? Inawezekana, kama haushiriki injili na wengine; kama hauhusiki katika kuwasaidia wengine waeneze injili.

Hauna sababu ya kuona haya; bado ni injili ile ile iliyo na uwezo wa kuokoa nafsi za wanadamu, ikifunua haki ya ajabu ya Mungu kuwaokoa wanadamu.

Tusije tukaona haya kwa ajili ya injili, au Yesu mwenyewe.

- Mk. 8:38, "*Maana kila mtu atakayenionea haya mimi, na maneno yangu katika kizazi hiki cha uzinzi na dhambi, Mwana wa Adamu atamwonea haya mtu huyo, atakapokuja katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika watakatifu.*"
- 1 Pet. 4:16, "*Lakini ikiwa kwa sababu ni Mkristo asione haya, bali amtukuze Mungu katika jina hilo.*"